

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 59 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** JANUARI 2026

KATIBU WA TUME AONGOZA KIKAO CHA MAANDALIZI YA BAJETI YA MWAKA 2026/2027



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akizungumza wakati wa kikao kazi cha maafisa bajeti wa Tume mjini Singida tarehe 12 Desemba, 2025.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

MWAKA MPYA 2026 UWE WA MAFANIKIO KATIKA MAENDELEO YA ELIMU

Tunapouanza mwaka mpya wa 2026, shule za msingi na sekondari nchini, isipokuwa kidato cha tano na sita, zinaanza muhula mpya wa masomo. Huu ni wakati muhimu wa kuanza upya kwa ari, mshikamano na dhamira ya kuimarisha ubora wa elimu kwa manufaa ya taifa na kizazi kijacho.

Tunawapongeza kwa dhati walimu wote kwa kazi kubwa na ya kujituma waliyoifanya katika mwaka 2025. Mchango wao umeendelea kuwa msingi wa mafanikio ya wanafunzi. Tunawahimiza katika mwaka 2026 kuendelea kufanya kazi kwa bidii, kuzingatia taratibu na maadili ya kazi, ili kuongeza kiwango cha ufaulu na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa wanafunzi, muhula mpya ni fursa mpya ya kujifunza kwa bidii na nidhamu. Tunawahimiza kuzingatia masomo yao kwa umakini, kuheshimu walimu na kuzingatia


kanuni za shule ili kufikia ustawi mzuri wa kitaaluma na kimaadili, ambao ni msingi wa mafanikio yao.

Aidha, tunawaomba wazazi na walezi kuendelea kudumisha ushirikiano na uhusiano mzuri na walimu pamoja na uongozi wa shule. Ushirikiano huu ni muhimu katika kufuatilia maendeleo ya wanafunzi na kutatua changamoto za kielimu kwa wakati, hivyo kuchangia maendeleo endelevu ya elimu.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) itaendelea kusimamia masuala ya ajira, maadili na maendeleo ya walimu ili kuhakikisha wanapata huduma bora na stahiki. Kwa mshikamano wa wadau wote, mwaka 2026 uwe mwaka wa mafanikio makubwa katika sekta ya elimu.

Kheri ya Mwaka Mpya!

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina M. Nkwama

Wajumbe
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera
Apsa Othman
Asha Lubuva

Mhariri Mkuu
Artemony T. Vincent

Mhariri
Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, S.L.P 353, DODOMA.



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

KATIBU WA TUME AONGOZA KIKAO CHA MAANDALIZI YA BAJETI YA MWAKA 2026/2027

Na Mwandishi Wetu, Singida.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, tarehe 12 Desemba 2025, ameongoza kikao kazi cha maafisa bajeti wa Tume mjini Singida ambacho ni sehemu ya maandalizi ya bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027.

Akizungumza katika kikao hicho, Mwl. Nkwama aliwapongeza maafisa hao kwa kazi wanayoifanya katika kuandaa bajeti hiyo huku akisema kuwa uadilifu na ubunifu wao ndiyo msingi mkubwa unaoiwezesha TSC kuendelea kuboresha huduma kwa walimu nchini.

“Ni muhimu bajeti tunayoiandaa iwe na tija na itakayoiwezesha Tume kutoa huduma bora kwa walimu wetu. Walimu wakipata huduma stahiki kwa wakati, wanafanya kazi kwa ufanisi na hatimaye ubora wa elimu nchini unaimarika,” alisema.

Ameongeza kuwa bajeti ya mwaka 2026/2027 ni lazima iendane moja kwa moja na Mpango Mkakati mpya wa Tume wa miaka mitano



Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Elia Malaki akitoa neno la utangulizi wakati wa kikao kazi cha maafisa bajeti wa Tume mjini Singida tarehe 12 Desemba, 2025.

(2026/27–2030/31) ili kuhakikisha kuwa vipaumbele, malengo na matokeo yanayotarajiwa yanaakisiwa kwenye utekelezaji wa kila mwaka.

Akizungumzia changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha, Mwl. Nkwama alisema Tume imeendelea kukutana na wadau mbalimbali ili kutafuta mbinu bora za kuongeza fedha za utekelezaji wa majukumu yake.

“Changamoto ya upungufu wa fedha linaendelea kufanyiwa kazi. Tume inaendelea kufanya majadiliano na wadau ili kuboresha upatikanaji wa fedha na kuhakikisha kuwa majukumu yetu yanatekelezwa kwa ufanisi,” alisisitiza.

Aidha, aliwataka watumishi na wataalam wote wa Tume kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na weledi ili kuiwezesha Serikali kutimiza dhamira yake ya kutoa huduma bora kwa wananchi, hususan walimu ambao ni nguzo muhimu katika sekta ya elimu.

Kikao kazi hicho kimehusisha maafisa bajeti kutoka idara na vitengo vya Tume Makao Makuu pamoja na maafisa kutoka ofisi za Tume ngazi ya Wilaya, ambapo washiriki walipata fursa ya kujadili vipaumbele, mikakati na mahitaji muhimu kwa ajili ya kuandaa bajeti yenye uhalisia na inayotekelezeka.



Washiriki wa kikao kazi cha maafisa bajeti wa Tume wakiwa kwenye kikao hicho tarehe 12 Desemba, 2025 mjini Singida.

KATIBU WA TUME AONGOZA KIKAO CHA MAANDALIZI YA BAJETI YA MWAKA 2026/2027



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama a k i z u n g u m z a wakati wa kikao kazi cha maafisa bajeti wa Tume mjini Singida tarehe 12 Desemba, 2025.



Washiriki wa kikao kazi cha maafisa bajeti wa Tume wakiwa kwenye kikao hicho tarehe 12 Desemba, 2025 mjini Singida.

**TSC BARIADI YAIMARISHA MASLAHI YA
WALIMU, MOTISHA YAONGEZEKA KAZINI**

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Bariadi, Wang'eng'i Mohabe, akiwa ofisini kwake.

Na Mwandishi Wetu, Bariadi

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bariadi, Mkoa wa Simiyu, imeendelea kupata mafanikio makubwa katika kuboresha maslahi ya walimu, hatua iliyochangia kuimarika kwa utendaji kazi, kuongezeka kwa motisha na kurejesha imani ya walimu kwa Tume hiyo.

Akizungumza katika mahojiano maalum na Jarida la Sauti ya TSC, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Bariadi, Wang'eng'i Mohabe, amesema maboresho yaliyofanyika kuanzia mwaka 2021 hadi 2025 yameleta mabadiliko chanya na yanayoonekana wazi katika sekta ya elimu wilayani humo.

**UPANDISHAJI MADARAJA
WAONDOA MALALAMIKO**

Mohabe amesema upandishaji wa madaraja kwa walimu umekuwa mojawapo ya mafanikio makubwa yaliyorejesha imani ya walimu kwa TSC.

"Hapo awali kulikuwa na malalamiko mengi, na mara nyingine tulionekana kama hatufanyi kazi. Kwa sasa hali imebadilika; tunapokutana

na walimu hata kwenye mikutano, wanatusikiliza na wanatuamini kwa sababu wameona changamoto zao zinapatiwa ufumbuzi," amesema Mohabe.

Kwa mujibu Mohabe, walimu wengi sasa wana ari ya kufanya kazi baada ya kuona juhudi zao zinatambuliwa na kuthaminiwa.

Mohabe amesema kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, walimu 3,077 wamepandishwa vyeo, wengi wao wakipandishwa zaidi ya mara moja kutokana na kutimiza vigezo na kufanya kazi kwa bidii.

Aidha, walimu 204 wamebadilishiwa muundo baada ya kujiendeleza kielimu, hatua iliyowapa nafasi ya kutumia taaluma zao ipasavyo na kuongeza tija katika sekta ya elimu.

**MIFUMO YA KIELEKTRONIKI
YARAHISISHA HUDUMA**

TSC Bariadi pia imenufaika na matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya kiutumishi, ambayo imeongeza uwazi na kupunguza ucheleweshaji wa huduma.

Mohabe amesema hapo awali kulikuwa na changamoto za barua kupotea, kuchelewa kupitishwa na

mabadiliko ya mishahara kuchelewa kutekelezwa.

"Kupitia mifumo ya sasa, mwalimu anaweza kuona hatua zote za ushughulikiaji wa suala lake, jambo lililoondoa malalamiko mengi," ameeleza.

**MABORESHO YA MISHAHARA
YAONGEZA HAMASA**

Mbali na upandishaji vyeo, maboresho ya nyongeza ya mishahara yameongeza hamasa kwa walimu na kuimarisha morali ya kufanya kazi kwa bidii, jambo linalochangia kuboresha ubora wa elimu kwa wanafunzi.

**CHANGAMOTO ZA ZAMANI
ZATATULIWA**

Akizungumzia changamoto zilizokuwepo awali, Mohabe amesema kulikuwa na utofauti wa vyeo kwa walimu wenye sifa sawa. Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kurekebisha hali hiyo kwa kuhakikisha kila mwalimu anawekwa katika cheo kinachostahili.

Kutokana na maboresho hayo, walimu 307 walipandishwa kwenye vyeo kinachofuata, huku walimu 20 wakipandishwa kwa msrerereko.

**MAADILI YA UTUMISHI
YAEENDELEA KUIMARIKA**

Mohabe amesema miongozo na kanuni mpya za utumishi wa umma zimewasaidia walimu kuelewa wajibu wao, haki zao na namna ya kuzifuatilia kwa kufuata taratibu.

"Hii imeimarisha nidhamu, maadili ya kazi na ufanisi katika utoaji wa elimu kwa wanafunzi," amesema.

USHAURI KWA WALIMU

Akitoa ushauri, Mohabe amewataka walimu kuepuka mikopo umiza, akisema imekuwa chanzo cha baadhi yao kukosa utulivu wa kufundisha na hata kuwa watoro.

Pia amewahimiza walimu kujiendeleza kielimu ili kuendana na mabadiliko ya elimu na kutoa elimu bora zaidi kwa wanafunzi, huku akisisitiza umuhimu wa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

"Taifa na jamii inawategemea walimu kuandaa kizazi kitakachosaidia Tanzania kupiga hatua zaidi za maendeleo," amehitimisha.

TSC BARIADI YAIMARISHA MASLAHI YA WALIMU, MOTISHA YAONGEZEKA KAZINI



Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Bariadi, Wange'ng'i Mohabe, akiwa ofisini kwake.



Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Bariadi, Wange'ng'i Mohabe (katikati), akiwa pamoja na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bariadi mara baada ya kikao cha kazi.

UTOAJI WA ELIMU YA MAADILI WASAIDIA KUPUNGUZA MAKOSA YA KINIDHAMU KWA WALIMU BUSEGA

Na Mwandishi wetu – Busega.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Busega imeendelea kuimarisha elimu ya maadili na usimamizi wa karibu kwa walimu, hali iliyosababisha kupungua kwa makosa ya kinidhamu na kuimarika kwa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

Akizungumzia suala la nidhamu, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Busega, Sylvester Itoba amesema kuwa TSC imeweka mkazo katika kutoa elimu badala ya adhabu tu. “Tumekuwa tukikutana na walimu katika kata na vituo vyao vya kazi ili kuwapa elimu ya maadili na sheria za utumishi wa walimu,” amesema.

Amesema kupitia elimu hiyo, makosa ya utoro kazini yamepungua kwa kiwango kikubwa. “Walimu waliokuwa wakikabiliwa na kosa la utoro walikuwa 28 mwaka 2016/2017, lakini kufikia mwaka 2024/2025 wamebaki walimu wanne pekee,” amesema Itoba.

Kwa upande wa vitendo vya ukiukwaji wa maadili kwa wanafunzi, Kaimu Katibu Msaidizi huyo amesema hali hiyo imedhibitiwa kabisa. “Katika wilaya ya Busega, vitendo vya mahusiano yasiyofaa kati ya walimu na wanafunzi vimeisha kabisa kutokana na usimamizi wa karibu na ushirikiano wa jamii ya shule,” ameeleza.

Kuhusu madai ya walimu, Kaimu Katibu Msaidizi amesema Serikali imeanzisha utaratibu wa kusikiliza na kushughulikia kero kupitia programu ya kliniki za kutakua changamoto za walimu. “Walimu walipewa fursa ya kuwasilisha madai yao kupitia kliniki ya Mama Samia, na madai halali yamekuwa yakilipwa kwa awamu,” amesema.

Akitoa ushauri kwa walimu, Kaimu Katibu Msaidizi amewataka kujiendeleza kitaaluma na kudumisha mahusiano mema na jamii. “Mwalimu anapokuwa na migogoro na jamii au uongozi wa shule, ufanisi wa elimu hupungua. Hivyo ni muhimu kudumisha mahusiano mema na kujiendeleza kielimu,” amesema.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Busega, Sylvester Itoba akiendelea kutekeleza majukumu ofisini kwake.

Amehitimisha kwa kusisitiza kuwa na jamii ndiyo msingi wa maendeleo ushirikiano kati ya Serikali, walimu endelevu ya elimu wilayani Busega.

SERIKALI IMEPANDISHA VYEO WALIMU WALIOSTAHILI WILAYANI SENGEREMA

Na Mwandishi Wetu – Sengerema

Buchosa.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya ya Sengerema imeishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutatua malalamiko ya walimu, hususan yale ya upandishwaji vyeo, kwa kuhakikisha walimu wote waliokidhi vigezo wanapatiwa haki zao kwa wakati.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Sengerema, Bw. Rhodes Hesron, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Makao Makuu ya Tume, yaliyofanyika ofisini kwake, kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

“Upandishwaji wa vyeo wilayani Sengerema unaendelea vizuri. Walimu wote wenye sifa wanapandishwa kwa wakati. Wachache ambao hawakupanda walikuwa na sababu mbalimbali ikiwemo mashauri ya kinidhamu, kuwa masomoni, likizo bila malipo au kutokufikisha viwango vya upimaji utendaji kupitia mfumo wa e-Utendaji,” alisema Bw. Hesron.

Alisema kuwa katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Desemba 2025, jumla ya walimu 3,499 wa shule za msingi na sekondari kutoka Halmashauri za Sengerema na Buchosa walipandishwa vyeo na madaraja. Aidha, walimu 162 walibadilishiwa muundo wa kiutumishi baada ya kujiendeleza kielimu.

Bw. Hesron alieleza kuwa hatua hiyo imewaongezea walimu ari ya kazi, kuwajengea moyo wa kujiendeleza kitaaluma na kuwaimarisha kiuchumi kupitia kuongezeka kwa viwango vya mishahara.

Aliongeza kuwa uboreshaji wa miundombinu ya elimu ikiwemo ujenzi wa shule mpya, madarasa na uwekaji wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) umechangia kupunguza umbali wa safari kwa walimu na wanafunzi, kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani na kuongeza ufaulu katika mitihani ya ndani na ya kitaifa.

Katika hatua nyingine, alisema kuwa utoaji wa Mwongozo kwa Walimu wa Ajira Mpya umeongeza uelewa wa masuala ya kiutumishi, maadili ya kazi na wajibu wa walimu, hali iliyosaidia kupunguza makosa ya kiutumishi.

Alibainisha kuwa kuanzia tarehe 04 hadi 07 Julai 2025, Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Sengerema iliendesha mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya, yaliyolenga kuwajengea uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu.

Kwa sasa, Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Sengerema inahudumia jumla ya walimu 4,070, wakiwemo 2,742 wa shule za msingi na 1,328 wa shule za sekondari kutoka Halmashauri za Sengerema na

WASEMAVYO WALIMU WA WILAYA YA SENGEREMA

Waipongeza Serikali kwa kutatua kero zao na kuboresha mazingira ya elimu

Baadhi ya walimu wa shule za msingi na sekondari wilayani Sengerema wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa jitihada kubwa za kutatua changamoto zao za muda mrefu, hususan masuala ya upandishwaji vyeo, miundombinu na matumizi ya TEHAMA katika sekta ya elimu.

Mwl. Nyema Baltazary Malale wa Shule ya Sekondari Igulumuki alisema Serikali imeboresha mazingira ya utoaji elimu kwa kuanzisha mifumo ya TEHAMA iliyopunguza safari za mara kwa mara na kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali. Aliongeza kuwa mitaala mipya imeongeza uelewa wa wanafunzi kwa njia ya vitendo badala ya kukariri.

Mwl. Auster Athanasio Bilalo wa Shule ya Msingi Sima alisema Serikali imeongeza vitendea kazi ikiwemo vitabu



Baadhi ya walimu wa Wilaya ya Sengerema wakiwa na Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

SERIKALI IMEPANDISHA VYEO WALIMU WALIOSTAHILI WILAYANI SENGEREMA

vya kiada na kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA ambayo imeokoa muda na kuongeza ufanisi wa kazi kwa walimu.

Mwl. Charles Mlelwa wa Shule ya Sekondari Ileanilo alisema mazingira ya ujifunzaji yameboreshwa kwa kuwezesha ufundishaji shirikishi unaowawezesha wanafunzi kujifunza kwa makundi, hali inayoongeza uelewa na kupunguza mzigo wa mwalimu.

Mwl. Robert Ramadhan Mussa wa Shule ya Sekondari Bitoto alisema mifumo ya TEHAMA imewawezesha walimu kupata taarifa, kutumia mifumo ya shule kama SIS, pamoja na kupata huduma za kifedha kupitia mfumo wa ESS kwa njia salama na rahisi.

Mwl. Maijo Musiba Magesa wa Shule ya Msingi Kamanga aliipongeza Serikali kwa kuboresha maslahi ya walimu kupitia nyongeza ya mishahara, malipo ya malimbikizo, ajira mpya na ujenzi wa miundombinu ya elimu ikiwemo madarasa na nyumba za walimu.

Walimu hao kwa pamoja waliomba Serikali kuendelea:

- Kuongeza idadi ya walimu,
- Kuboresha miundombinu ya shule,
- Kupanua matumizi ya TEHAMA,
- Kuajiri wataalamu wa masomo maalumu na TEHAMA mashuleni,
- Kuboresha upatikanaji wa umeme na maji shuleni.



Baadhi ya walimu wa Wilaya ya Sengerema wakiwa na Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

TSC WILAYA YA MEATU YAONESHA MAFANIKIO KATIKA KUBORESHA MASLAHI YA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Meatu

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Meatu imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio katika kusimamia masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Meatu, Afisa wa TSC, Bw. Josephat Msonge, amesema kuwa katika kipindi cha hivi karibuni, TSC imefanikiwa kutekeleza upandishaji wa madaraja kwa walimu wa shule za msingi na sekondari, kuwabadilishia vyeo na miundo ya kazi, pamoja na kushughulikia taratibu za walimu wapya kazini.

Ameeleza kuwa Serikali pia imeendelea kulipa malimbikizo ya mishahara, fedhazali kizio na gharama za matibabu kwa walimu, hatua ambayo imechangia kuboresha ustawi wao na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kielimu.

Kuhusu changamoto zilizokuwepo awali, amesema kuwa ucheleweshaji wa upandishaji madaraja na ulipaji wa madai ulikuwa changamoto kubwa, lakini Serikali ya Awamu ya Sita imechukua hatua madhubuti kuyatatua na kufanikiwa kuondoa malalamiko yaliyokuwepo kwa muda mrefu.

Bw. Msonge aliongeza kuwa miongozo iliyotolewa hivi karibuni imewasaidia walimu kufahamu haki na wajibu wao, kuzingatia maadili ya utumishi, kufuata taratibu, kutunza siri za Serikali na kutafuta ufumbuzi wa masuala yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Ameeleza kuwa elimu ya kiutumishi hutolewa kwa walimu kupitia vikao, semina, warsha, mikutano na makongamano ya walimu, hali iliyosaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa makosa ya kinidhamu kama utoro, uchelewaji kazini, migogoro mahali pa kazi,



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu katika Wilaya ya Meatu, Bw. Josephat Msonge akiendelea kutekeleza majukumu ofisini kwake.

ukaidi na mahusiano yasiyofaa kati ya walimu na wanafunzi.

SERIKALI YAPANDISHA VYEO WALIMU 3,385 KATIKA WILAYA YA ILEMELA

Na Mwandishi Wetu – Ilemela

Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepandisha vyeo walimu 3,385 wa shule za umma katika Wilaya ya Ilemela, mkoani Mwanza, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ilemela, Bw. Yonas Alfred Maduhu, alipokuwa akielezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa majukumu yake.

Bw. Maduhu alisema kuwa kati ya walimu hao waliopandishwa vyeo, 1,945 ni wa shule za msingi na 1,440 wa shule za sekondari. Aidha, alisema kuwa walimu 556 walibadilishiwa vyeo baada ya kujiendeleza kielimu.

“Upandishaji wa vyeo na madaraja kwa walimu ni mzuri kwani walimu wote waliokuwa na sifa za kupandishwa au kubadilishiwa vyeo walipata haki zao,” alisema.

Aliongeza kuwa juhudi hizo za Serikali ya Awamu ya Sita zimeondoa changamoto iliyokuwepo kwa muda mrefu ya walimu kuchelewa kupandishwa madaraja na kuachwa na walimu walioajiriwa nao kwa wakati mmoja.

Bw. Maduhu alisema kuwa hali ya ufundishaji imeendelea kuimarika baada ya Serikali kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, ikiwemo ujenzi wa madarasa, ofisi, utekelezaji wa mpango wa Shule Salama, pamoja na matumizi ya Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), hali iliyorahisisha ufundishaji na ujifunzaji.

Aidha, aliishukuru Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu kwa kutoa miongozo mbalimbali iliyowasaidia walimu kupata elimu ya kiutumishi na kujiepusha na vitendo vinavyoshusha hadhi ya taaluma ya ualimu, ikiwemo ulevi, utoro na ukaidi kazini.

Alisema kuwa hatua hiyo imewawezesha walimu kutambua wajibu wao wa kiutumishi na kupunguza migogoro baina yao na wasimamizi wa vituo vya kazi, hali iliyosababisha Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Ilemela kutopokea malalamiko yoyote ya utovu wa nidhamu kwa walimu wapya.



Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ilemela, Bw. Yonas Alfred Maduhu

Bw. Maduhu aliongeza kuwa Tume imekuwa ikitoa elimu ya mara kwa mara kwa walimu kwa kutumia miongozo na vipeperushi vinavyosambazwa katika shule mbalimbali ili kuwawezesha kufahamu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wao.

Alisema elimu hiyo pia inahusisha kuwahamasisha walimu kuepuka mikopo umiza au kausha damu na badala yake kuelekezwa kwenye taasisi rasmi na salama za kifedha ili kuepuka vitendo vinavyoweza kudhalilisha taaluma ya ualimu.

WASEMAVYO WALIMU WA WILAYA YA ILEMELA

Baadhi ya walimu wa Wilaya ya Ilemela wamepongeza jitihada za Serikali katika kuboresha maslahi yao na kutatua changamoto zinazowakabili.

MWL. ABEDNEGO MARCO BUSHINI – SHULE YA MSINGI BUYOMBE

“Jitihada za Serikali za kuboresha maslahi ya walimu ni kubwa ikilinganishwa na kipindi cha nyuma, hususan kupitia Mfumo wa Upimaji Utendaji wa Watumishi (e-Watumishi).”

Aliiomba Serikali kuendelea kutoa semina elekezi za mara kwa mara kwa walimu ili ziwawezeshe kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia. Pia aliishukuru Serikali kwa kuanzisha matumizi ya TEHAMA shuleni, hali iliyorahisisha utekelezaji wa majukumu kwa haraka na kwa gharama nafuu, pamoja na kuanzishwa kwa mitaala mipya inayotoa motisha kupitia mafunzo endelevu.

MWL. YANIPHA ELIAZARY – SHULE YA SEKONDARI BUGONGWA

Aliomba Serikali kuendelea kuboresha maslahi ya walimu kwa kuwapandisha madaraja waliokidhi vigezo, kuongeza mishahara na kutoa motisha kwa walimu wanaofanya vizuri.

Aliishukuru Serikali kwa kuwawezesha walimu kupata kompyuta zilizorahisisha maandalizi ya ufundishaji na upatikanaji wa nyaraka muhimu, pamoja na kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA shuleni na kutoa semina elekezi za mara kwa mara.

MWL. EVARIST ZACHARIA KELEGE – SHULE YA WASICHANA BWIRU

“Jitihada za Serikali za kuboresha maslahi ya walimu ni nzuri, na ningeshauri Serikali kuendelea kuwajali walimu kwa kuhakikisha wanapandishwa vyeo kwa wakati, na waliochelewa kufanyiwa mpango wa mserereko.”

Aliishukuru Serikali kwa matumizi ya TEHAMA shuleni na kuanzishwa kwa mitaala mipya inayotumia vitendo zaidi kuliko nadharia, hali iliyopunguza mzigo wa kazi kwa walimu na kuongeza uelewa kwa wanafunzi.

MWL. CHACHA WILLISON MASWE – SHULE YA MSINGI BEZI

“Serikali imejitahidi kuongeza mishahara ya walimu jambo lililoborahisha maisha yetu, na upandishaji vyeo umeongeza maslahi na ari ya kazi.”

Aliishukuru Serikali kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu ikiwemo madarasa na nyumba za walimu, pamoja na kuanzisha mitaala mipya na matumizi ya TEHAMA yaliyorahisisha uhifadhi wa kumbukumbu na kuokoa muda.

MWL. MAKOYE MAGEGE SAMBE – SHULE YA MSINGI KITANGIRI C

“Jitihada za Serikali katika kutatua kero za walimu ni nzuri na zinaonekana kwa vitendo.”

Aliiomba Serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu ikiwemo madarasa, ofisi na nyumba za walimu. Pia aliishukuru Serikali kwa mitaala mipya na matumizi ya TEHAMA ambayo yameongeza uelewa kwa wanafunzi na kuwawezesha walimu kufundisha mada zinazoendana na mazingira halisi ya sasa.

JITIHADA ZA SERIKALI ZAZAA MATUNDA KWA WALIMU BUSEGA

**WALIMU WASEMA MABORESHO
YAMEONGEZA ARI YA KAZI NA
KUINUA UFAULU WA WANAFUNZI**



*Samwel Nasson Erasto wa Shule ya Sekondari Mwaniga
iliyopo Wilaya ya Busega.*

Na mwandishi wetu – Busega, Simiyu.

Walimu katika Wilaya ya Busega wameeleza kuridhishwa na jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha maslahi na mazingira ya kazi, wakisema hatua hizo zimeongeza morali, bidii na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Akizungumza katika mahojiano maalum, Mwl. Samwel Nasson Erasto, anayefundisha masomo ya Fizikia na Hisabati katika Shule ya Sekondari Mwaniga, amesema Serikali imefanya mageuzi makubwa yenye tija kwa walimu tangu kuingia madarakani.

“Kwa miaka saba niliyokaa katika taaluma ya ualimu, Awamu ya Sita imeonyesha dhamira ya dhati kwa walimu. Mishahara imeboreshwa, madeni na malimbikizo yanalipwa kwa wakati, walimu wamepandishwa madaraja na ajira mpya hasa za masomo ya sayansi zimetupunguzia mzigo wa kazi,” amesema Mwl. Samwel.

MABORESHO YAONGEZA ARI KAZINI

Kwa mujibu wa Mwl. Samwel, maboresho hayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa ari, nguvu na bidii kazini, hali inayojidhihirisha katika maandalizi ya vipindi, ufundishaji darasani na ufuatiliaji wa maendeleo ya wanafunzi.

Ameongeza kuwa mazingira ya kazi katika shule nyingi yanaendelea kuimarika ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Akitolea mfano shule anayofundisha, amesema licha ya kuwa ni shule mpya, tayari imepokea fedha za mradi wa EP4R kwa ajili ya ujenzi wa vyoo, hatua



*Mkuu wa Shule ya Msingi Itongo- Busega, Mwl. Saire
Joseph Wandwi.*

inayosaidia kuboresha afya na ustawi wa wanafunzi na walimu.

MIUNDOMBINU, KICHOCHEO CHA UFAULU

Akizungumzia mchango wa miundombinu na vifaa vya kufundishia, Mwl. Samwel amesema vina nafasi kubwa katika kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

“Miundombinu bora na vifaa vya kufundishia huleta matokeo chanya moja kwa moja. Tunaomba Serikali iendeele kuboresha sekta ya elimu kadri itakapopata nafasi,” amesema.

Pia ameshauri Serikali kuanzisha mitihani ya vitendo (practical) kwa wanafunzi kuanzia kidato cha kwanza ili kuwajengea uelewa wa kina wa masomo ya sayansi mapema.

MAADILI YA WALIMU NI MSINGI WA ELINU BORA

Mwl. Saire Joseph Wandwi, Mkuu wa Shule ya Msingi Itongo wilayani Busega, amesema kuwa mwalimu ni kioo cha jamii, hivyo nidhamu na maadili ni jambo lisilojadiliwa.

Ameeleza mbinu wanazotumia kuhakikisha walimu wanazingatia maadili ya kazi, kuwa ni pamoja na:

Kukaa vikao vya walimu na kuwaeleza wazi athari za kukiuka maadili ya taaluma ya ualimu, kuwaita ofisini walimu wanaoonekana kwenda kinyume na maadili na kuwapa maelekezo na ushauri wa moja kwa moja na kutoa ushauri wa mara kwa mara na kuwakumbusha walimu dhamana waliyopewa na Taifa ya kutoa elimu bora kwa watoto.

“Taaluma ya ualimu ni wito. Tunapaswa kuilinda kwa vitendo na maamuzi yetu ya kila siku,” amesisitiza Mwl. Wandwi.

HITIMISHO

Kauli za walimu wilayani Busega zinaonesha wazi kuwa jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita zimeleta matumaini mapya katika sekta ya elimu. Maboresho ya maslahi, mazingira ya kazi na miundombinu yanaendelea kuwa chachu ya elimu bora na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

SERIKALI YAPANDISHA VYEO WALIMU 2,491 WILAYANI KWIMBA

Na Mwandishi Wetu – Kwimba

Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepandisha vyeo walimu wa shule za umma 2,491 wilayani Kwimba katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kwimba, Bw. Mwita Silas Gisiri, alipokuwa akielezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa majukumu yake.

Alisema kati ya walimu hao, 1,533 ni wa shule za msingi na 958 ni wa shule za sekondari, huku walimu 192 wakibadilishiwa muundo baada ya kujiendeleza kielimu.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kwimba, Bw. Mwita Silas Gisiri, akizungumza na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini ofisini kwake kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.

“Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, walimu wote wenye sifa wamepandishwa vyeo. Hatua hii imeongeza morali na ari ya kufanya kazi, hali iliyochangia kuongezeka kwa ufaulu wa Mtihani wa Darasa la Saba mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 93.4, ukilinganishwa na asilimia 86.1 mwaka 2024,” alisema Bw. Gisiri.

Aliongeza kuwa juhudi hizo zimeondoa changamoto ya walimu waliokuwa na sifa kuchelewa kupandishwa madaraja.

Aidha, aliishukuru Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu kwa kutoa miongozo mbalimbali iliyowasaidia walimu kupata elimu ya kiutumishi, jambo lililopunguza vitendo vinavyoshusha hadhi ya taaluma ya ualimu kama vile ulevi, utoo na ukaidi.

Kwa mujibu wa Bw. Gisiri, mashauri ya kinidhamu yameendelea kupungua kila mwaka ambapo mwaka 2023/2024 yalikuwa 17, mwaka 2024/2025 yalipungua hadi 15, na mwaka 2025/2026 yamefikia 11.

Alisema miongozo hiyo imewawezesha walimu kufanya kazi kwa bidii, kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wao, hivyo kuinua kiwango cha elimu kwa wanafunzi.

“Mwongozo mpya wa ajira umewasaidia walimu kuelewa maadili ya kazi zao, wajibu wao na namna ya kudai haki zao, hali inayowasaidia kujiepusha na makosa ya kiutumishi,” aliongeza.

Alifafanua kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kwimba, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, imekuwa ikiendesha vikao vya mara kwa mara na walimu pamoja na wakuu wa shule kwa lengo la kuwahamasisha kuzingatia sheria na taratibu ili kuepuka mashauri ya kinidhamu.

Hatua hiyo, alisema, imeimarisha nidhamu na ushirikiano kati ya walimu, wazazi, Ofisi ya TSC na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba.

Kufikia Desemba 2025, Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kwimba inahudumia walimu 2,408, wakiwemo 1,608 wa shule za msingi na 800 wa shule za sekondari, waliopo katika shule 157 za msingi na shule 41 za sekondari.

WASEMAVYO WALIMU WA WILAYA YA KWIMBA

Baadhi ya walimu wa Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza wamepongeza jitihada za Serikali katika kuboresha maslahi yao na kutatua changamoto zinazowakabili.

Mwl. Mpemba Mathias Nkwabi, Mwalimu wa Shule ya Msingi Bugembe, alisema Serikali imefanikiwa kuboresha maslahi ya walimu na mazingira ya utoaji elimu, hali inayowezesha walimu kupanda madaraja kwa wakati na kufanya kazi kwa ufanisi.

Aliomba Serikali kuboresha ikama ya walimu hasa katika shule za vijijini kutokana na ongezeko la wanafunzi ikilinganishwa na idadi ya walimu waliopo.

Mwl. Emmanuel Kashasha, Mwalimu wa Shule ya Msingi Welamasonga, aliipongeza Serikali kwa kuboresha maslahi ya walimu, kuongeza mishahara, kutoa motisha, kujenga madarasa, nyumba za walimu na kusambaza vitabu vya kiada.

Alisema matumizi ya mifumo ya TEHAMA shuleni yamerahisisha utendaji kazi, upatikanaji wa taarifa, nyaraka, stahiki za walimu kupitia mfumo wa e-Watumishi pamoja na huduma za kifedha.

Mwl. Joseph Kangati Henry, Mwalimu wa Shule ya Msingi Mwalubungwe, alisema uboreshaji wa miundombinu na mazingira ya kufundishia umechangia kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi na idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa darasa la awali na la kwanza.

Aliomba Serikali kuongeza idadi ya walimu na kuendelea na ujenzi wa nyumba za walimu ili kuboresha zaidi mazingira ya kazi.

SERIKALI YAPANDISHA VYEO WALIMU 2,591 WILAYANI KWIMBA



Mwl. Joseph Kangati Henry



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume
ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya
Kwimba, Bw. Mwita Silas Gisiri



Mwl. Mpemba Mathias Nkwabi

MWL. MAYAU AKOSHWA NA JITIHADA ZA SERIKALI KUBORESHA MASLAHI YA WALIMU

Na Mwandishi Wetu, Meatu

M WALIMU wa Shule ya Msingi Itongolyangamba iliyopo Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu, Bw. Masigati Peter Mayau, ameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuboresha maslahi ya walimu na mazingira ya kazi katika sekta ya elimu.

Akizungumza na Sauti ya TSC hivi karibuni, Mwl. Mayau ambaye ana uzoefu wa miaka 21 katika taaluma ya ualimu, amesema Serikali imeonesha dhamira ya dhati ya kuwajali walimu kupitia utekelezaji wa mikakati mbalimbali ikiwemo nyongeza za mishahara, upandishaji wa madaraja, ubadilishaji wa miundo ya kazi pamoja na ulipaji wa madai ya walimu.

“Serikali ya Awamu ya Sita imeonyesha dhamira ya dhati kwa walimu kupitia nyongeza za mishahara, upandishaji wa madaraja, ubadilishaji wa miundo ya kazi pamoja na ulipaji wa madai mbalimbali,” amesema.

Ameeleza kuwa maboresho hayo yameleta tija siyo tu kazini bali pia katika maisha binafsi ya walimu. Amesema yeye ni miongoni mwa walimu walionufaika na maboresho hayo baada ya kupandishwa madaraja na kubadilishiwa muundo wa kazi.

“Maboresho haya yamenisaidia kuboresha maisha yangu na ya familia yangu pamoja na kupunguza msongo wa mawazo katika utekelezaji wa majukumu ya kazi,” ameeleza.

Hata hivyo, Mwl. Mayau ameshauri Serikali kuendelea kushirikisha wadau wa elimu kuanzia ngazi ya chini kabla ya utekelezaji wa sera na mipango ya elimu, pamoja na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Pia amesisitiza umuhimu wa kuwapatia walimu mafunzo ya mara kwa mara ili kuendana na mabadiliko ya mitaala.

Akizungumzia suala la nidhamu na maadili kazini, amesema uongozi wa shule kwa kushirikiana na mamlaka husika unaendelea kusimamia maadili ya walimu kwa kutoa elimu ya sheria, kanuni na taratibu za utumishi pamoja na kuimarisha mahusiano mema kati ya walimu, wanafunzi, jamii na viongozi.

Amehitimisha kwa kusema kuwa ushirikiano mzuri uliopo kati ya uongozi wa shule na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) umechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha nidhamu, uwajibikaji na ufanisi kazini.

“Ushirikiano kati ya uongozi wa shule na Tume ya Utumishi wa Walimu umechangia kwa kiasi kikubwa kudumisha nidhamu, uwajibikaji na ufanisi katika utendaji kazi wa walimu,” amesema.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Itongolyangamba iliyopo Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu, Masigati Peter Mayau akiendelea na majukumu ya kazi ofisini kwake.

SERIKALI YATATUA KERO ZA WALIMU WILAYANI MISUNGWI

Na Mwandishi Wetu – Misungwi

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Misungwi imesema Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikiwa kutatua kero mbalimbali za walimu kwa kuwapandisha vyeo, kubadilisha miundo ya kiutumishi na kulipa stahili zao kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni na Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Misungwi, Bw. Manyanza John Mageme, alipokuwa akielezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa majukumu yake.

Bw. Mageme alisema kuwa katika kipindi hicho, walimu 2,554 walipandishwa vyeo, wakiwemo 1,776 wa shule za msingi na 778 wa shule za sekondari. Aidha, walimu 180 walibadilishiwa muundo wa kiutumishi baada ya kujiendeleza kielimu, ambapo 158 ni wa shule za msingi na 28 wa shule za sekondari.

Aliongeza kuwa Serikali imelipa jumla ya shilingi milioni 852.5 ikiwa ni malipo ya likizo, huku walimu 875 wa shule za msingi na sekondari wakilipwa malimbikizo ya mishahara.

Aidha, alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Misungwi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imefanikiwa kufanya ziara katika shule mbalimbali kwa lengo la kuwaelimisha walimu kuhusu umuhimu wa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu ili kuepuka makosa yanayoweza kuhatarisha ajira zao.

“Tumekuwa tukifanya ziara za kikazi shuleni kuwakumbusha walimu kuhusu maadili ya taaluma, wajibu wao kwa wanafunzi, waajiri na jamii pamoja na haki na stahili zao, ili wajiepushe na makosa yanayoweza kuhatarisha utumishi wao,” alisema Bw. Mageme.

Alifafanua kuwa katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025, Tume imewafikia walimu 2,350, wakiwemo 1,645 wa shule za msingi na 715 wa shule za sekondari. Vilevile, elimu ya kiutumishi imetolewa kwa wakuu

wa shule 186, kati yao 41 wa shule za sekondari na 145 wa shule za msingi, ili kuwawezesha kutekeleza vyema majukumu yao kama mamlaka ya nidhamu kwa walimu wanaowasimamia.

Bw. Mageme alisema kuwa lengo la jitihada hizo ni kuzuia walimu kujiingiza katika makosa ya kiutumishi kama vile utoro wa rejareja na wa kudumu, ulevi, mahusiano yasiyofaa na wanafunzi pamoja na ukaidi, ambayo yote yanahatarisha ajira zao.

“Serikali inawekeza fedha nyingi

katika kuwaandaa walimu kwa sababu wanahusika moja kwa moja katika kuandaa rasilimali watu wa sekta mbalimbali. Ndiyo maana sisi kama Tume wilayani Misungwi tunatumia muda mwingi kuwaelimisha walimu kuhusu wajibu wao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu ili wasipoteze fursa na uwekezaji mkubwa uliowekwa na Serikali,” alisisitiza.

Katika hatua nyingine, alisema Mwongozo wa Waajiriwa Wapya uliotolewa umewezesha walimu wapya na waliopo kazini kupata



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Misungwi Manyanza John Mageme akizungumza na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wakati akielezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi cha maika minne iliyopita ya utekelezaji wa majukumu yake.

SERIKALI YATATUA KERO ZA WALIMU WILAYANI MISUNGWI

uelewa mpana wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazoongoza utumishi wao, pamoja na haki na wajibu wao katika utekelezaji wa majukumu.

"Mwongozo huu umekuwa muhimu hasa kwa waajiriwa wapya ambao walikaa muda mrefu nje ya mfumo wa ajira, kwani umewakumbusha misingi ya maadili na wajibu wao kama walezi wa watoto wakiwa shuleni," aliongeza.

Alisema mwongozo huo pia umewasaidia wadau wengine wakiwemo madiwani kuelewa vyema majukumu, haki na wajibu wa walimu kwa mujibu wa Sheria.

WALIMU WAIPONGEZA SERIKALI

Kwa upande wake, Mwl. Jackson Henry Kasuluja wa Shule ya Msingi Kibula alisema Serikali imejitahidi kwa kiwango kikubwa kutatua changamoto za walimu tangu ilipoingia madarakani.

Alisema walimu waliokuwa wamecheleweshewa madaraja wamepandishwa, waliobadilisha sifa wamebadilishiwa miundo ya kiutumishi na posho mbalimbali ikiwemo nauli za likizo zimelipwa.

Mwl. Kasuluja aliongeza kuwa miongozo iliyotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu imewasaidia walimu kujitambua vyema kuhusu haki na wajibu wao kwa mwajiri, wanafunzi na jamii, hali iliyowasaidia

kujiepushana makosayanayopelekea mashauri ya kinidhamu.

Aliipongeza Serikali kwa kuanzisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA shuleni, hatua iliyorahisisha ufundishaji, kuongeza ushirikishwaji wa wanafunzi na kuboresha ufaulu.

Aliiomba Serikali kuendelea kuongeza idadi ya walimu, kuboresha nyumba za walimu, kupanua matumizi ya TEHAMA na kuajiri wataalamu wa masomo maalumu kama sanaa na michezo. Aidha, aliipongeza Serikali kwa uanzishaji wa mitaala mipya inayowawezesha walimu kutumia mbinu bunifu katika ufundishaji.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Misungwi Manyanza John Mageme (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mwalimu wa Shule ya Msingi Ng'ombe Mwl Tingu Kapaya Mbole (wa pili kutoka kulia), Mwalimu wa Shule ya Msingi Nange Mwl. Abdala Ahmed Mimi (kulia), Mwalimu wa Shule ya Msingi Bugisha Mwl. Masanja Michael Shija (kushoto) na Mwalimu wa Shule ya Kibula Jackson Henry Kasuluja (wa pili kutoka kushoto) mara baada ya kuzungumza hivi karibuni na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi cha maika minne iliyopita ya utekelezaji wa majukumu yake.

UTOAJI WA ELIMU YA MAADILI WASAIDIA KUPUNGUZA MAKOSA YA KINIDHAMU KWA WALIMU BUSEGA

Na Mwandishi wetu – Busega.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Busega imeendelea kuimarisha elimu ya maadili na usimamizi wa karibu kwa walimu, hali iliyosababisha kupungua kwa makosa ya kinidhamu na kuimarika kwa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

Akizungumzia suala la nidhamu, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Busega, Sylvester Itoba amesema kuwa TSC imeweka mkazo katika kutoa elimu badala ya adhabu tu. “Tumekuwa tukikutana na walimu katika kata na vituo vyao vya kazi ili kuwapa elimu ya maadili na sheria za utumishi wa walimu,” amesema.

Amesema kupitia elimu hiyo,

makosa ya utoro kazini yamepungua kwa kiwango kikubwa. “Walimu waliokuwa wakikabiliwa na kosa la utoro walikuwa 28 mwaka 2016/2017, lakini kufikia mwaka 2024/2025 wamebaki walimu wanne pekee,” amesema Itoba.

Kwa upande wa vitendo vya ukiukwaji wa maadili kwa wanafunzi, Kaimu Katibu Msaidizi amesema hali hiyo imedhibitiwa kabisa. “Katika wilaya ya Busega, vitendo vya mahusiano yasiyofaa kati ya walimu na wanafunzi vimeisha kabisa kutokana na usimamizi wa karibu na ushirikiano wa jamii ya shule,” ameeleza.

Kuhusu madai ya walimu, Itoba amesema Serikali imeanzisha utaratibu wa kusikiliza na kushughulikia kero kupitia programu

ya kliniki za kutakua changamoto za walimu. “Walimu walipewa fursa ya kuwasilisha madai yao kupitia kliniki ya Mama Samia, na madai halali yamekuwa yakilipwa kwa awamu,” amesema.

Akitoa ushauri kwa walimu, Kaimu Katibu Msaidizi amewataka kujiendeleza kitaaluma na kudumisha mahusiano mema na jamii. “Mwalimu anapokuwa na migogoro na jamii au uongozi wa shule, ufanisi wa elimu hupungua. Hivyo ni muhimu kudumisha mahusiano mema na kujiendeleza kielimu,” amesema.

Amehitimisha kwa kusisitiza kuwa ushirikiano kati ya Serikali, walimu na jamii ndiyo msingi wa maendeleo endelevu ya elimu wilayani Busega.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Busega, Sylvester Itoba akiendelea kutekeleza majukumu ofisini kwake.

WALIMU 6,669 WA WILAYA YA NYAMAGANA WAPANDISHWA VYEO KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE

Na Mwandishi Wetu – Nyamagana

Jumla ya walimu 6,669 wa shule za umma katika Wilaya ya Nyamagana, mkoani Mwanza, wamepandishwa vyeo na Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nyamagana, Bi. Victoria Rugaba, alipokuwa akielezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa majukumu yake.

Bi. Rugaba alisema kuwa kati ya walimu hao waliopandishwa vyeo, 4,184 ni wa shule za msingi na 2,485 ni wa shule za sekondari.

"Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tangu aingie madarakani amejitahidi kwa dhati kutatua changamoto za walimu. Kwa sasa hali ya upandishaji vyeo ni nzuri ukilinganishwa na miaka ya nyuma, kwani

walimu wote waliokidhi vigezo wamepandishwa vyeo," alisema.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho, walimu 468 walibadilishiwa miundo ya kiutumishi baada ya kujiendeleza kielimu, ambapo 344 ni wa shule za msingi na 124 wa shule za sekondari.

Aidha, Bi. Rugaba aliishukuru Serikali kwa kuwezesha kutolewa kwa Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wa Ajira Mpya, ambao umesaidia kuwajengea walimu uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu pamoja na Maadili yanayosimamia utumishi wao.

Alisema kupitia mwongozo huo, walimu wamepata uelewa wa taratibu za ajira na maendeleo ya kazi ikiwemo uthibitisho kazini, upandishwaji vyeo, pamoja na uchaguzi wa kozi za kujiendeleza kielimu.

"Mwongozo huu pia umesaidia walimu kuelewa taratibu za mawasiliano Serikalini na namna ya kushughulikia malalamiko yao, jambo ambalo limesababisha kupungua kwa idadi ya malalamiko," alieleza.

Katika hatua nyingine, Bi. Rugaba alisema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Nyamagana imekuwa ikitumia mbinu mbalimbali kuhakikisha walimu wanaendelea kuwa mfano bora katika jamii kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Maadili, ikiwemo kufanya ziara za mafunzo shuleni.

Aliongeza kuwa Tume imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Mafisa Udhubiti Ubora wa Shule na Mafisa Elimu wa shule za msingi na sekondari kuendesha semina za elimu ya kiutumishi kwa walimu.

Wakati huo huo, aliishukuru Serikali kwa kuwezesha upatikanaji wa gari la kazi, ambalo limewawezesha maafisa wa Tume kuwafikia walimu kwa urahisi zaidi wanapotoa elimu kuhusu uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Maadili ya Utumishi wa Walimu.

Kwa sasa, Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Nyamagana inahudumia jumla ya walimu 4,008, wakiwemo 2,481 wa shule za msingi na 1,527 wa shule za sekondari, wanaofundisha katika shule 88 za msingi na shule 35 za sekondari.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nyamagana, Bi. Victoria Rugaba



MWAKA HUU
UTAKUWA WA
MAFANIKO ZAIDI
ASANTE KWA
KUTUONGOZA
VIZURI!

HONGERENI
SANA
KWA KAZI
KUBWA NA
KUJITUMA
MWAKA
ULIOPITA
2025

ELIMU

2026

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz